بسم الله الرحمن الرحيم

Ijumaa07/Rabiul Awwal/1428 H =26/03/2007 AD,Pongwe-Tanga,Tanzania.makala namba 13.

# HII NDIYO DAAWA YETU

# JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

SHEIKH DKT. RABII AL MAD KHALY BAINA YA MTAZAMO WA MAULAMAA WA SUNNA NA WAZUSHI

**قال الإمام العلامة محدث العصر محمد ناصر الدين الألباني:**
**أقول: إن حامل راية الجرح والتعديل اليوم فى العصر الحاضر وبحق هو أخونا الدكتور ربيع،والذين يردون عليه لا يردون بعلم أبداً والعلم معه..**

**Amesema sheikh al Bany;**
**Ninasema kwamba;aliyebeba bendera ya Jarhu wa Ta'adil katika zama za leo tena kwa haki ni ndugu yetu Dkt Rabii.Na wale wanaompinga,daima hawampingi kwa elimu,na elimu ipamoja na Rabii..**
**Tazama kitabu at thanaaul badi'u uk 18.**

MUANDISHI;

AL AKH ABUL FADH'LI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote.
Ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya utangulizi wa kheri na baraka,kwa lengo la kutaka kuelimisha,na kubainisha ukweli,jambo ambalo mimi ninalihisi kuwa ni wajibu wangu hasa katika wakati huu ambao wamekithiri wapotoshaji wa haki.

Na miongoni mwa mambo muhimu ya kubainishwa ni kuwafahamisha watu hasa wale wenye kufuata Sunna za Mtume s.a.w.na kujinasibisha na njia ya Salaf Swalih nalo ni suala zima la kuwajua maulamaa wa kuwarejea wakati inapobidi kufanya hivyo.

Na miongoni mwa maulamaa hao waliokuwa katika mstari wa sawasawa,na njia iliyonyooka kwa ushuhuda wa maulamaa wakubwa wa zama hizi ni Sheikh al allaama Dkt Rabii Ibn Haady Ibn Umayr al Mad'khaly.

## NINANI SHEIKH RABII?

Kwanza kabisa kuna umuhimu wa kuielezea historia yake kwa ufupi;

1- Jina lake kamili ni;Rabii Ibn Haady Ibn Umayr al Mad khaly.
2- Alipozaliwa; amezaliwa katika kijiji cha al Juradiyya sehemu za Swaamitwa kusini mwa Saudi Arabia.
3- Mwaka aliozaliwa;1351 Hijiriya.
4- Aliposoma ;kwanza alisoma huko kwao,kisha alijiunga na al Ma'ahad al il my huko huko kwao,kisha Chuo kikuu cha Madina na alimaliza masomo ya shahada ya kwanza mwaka 1385 hijiriya,na kuchukua shahada ya pili 1396 h,kisha Phd katika chuo kikuu cha King Abdul Aziz kilichopo Jeddah.na amesoma katika msikiti wa Mtume s.a.w. kwa Sheikh Ibn Baaz,na amesuhubiana na Sheikh Al bany kwa muda mrefu,na Sheikh Hammad al Ansaary,na wengineo katika maulamaa wakubwa.

5- Kazi zake;aliwahi kuwa muwakilishi wa chuo kikuu cha Madina kule India,na aliwahi kuwa ni mkuu wa kitengo cha Sunna katika chuo kikuu cha Madina mpaka alipohama Madina kwenda Makka kwasababu za kiafya.

## KWANINI TUNAMZUNGUMZIA SHEIKH RABII?

Hili ni swali zuri na muhimu,tumeamua kumzungumzia mwanawachuoni huyu wa ahli sunna katika zama hizi kwasababu kuu zifuatazo;
1-Kutokufahamika kwa maulamaa wengi wa Sunna mmoja wapo ni huyu Sheikh Rabii.

2-maneno ya watu wa bid'a dhidi yake.

3-upotoshaji wa haki dhidi ya Sheikh huyu uliofanywa na Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga Sheikh Salim Barahiyan katika muhadhara wake aliokuwa akizungumzia kuhusa Salafiyya Jadidah! Pale alipodai kwamba kuna kundi potofu linaloitwa Salafiyya Jadida kundi ambalo limeanzishwa na masheikh hawa;

Rabii al Mad khaly
Muq bil Ibn Haady al Waadi'y
Pamoja na Yahya Ibn Ally al Hajuury mwanafunzi wa Sheikh Muqbil.

Suala la Salafiyya Jadida kuwepo kwake na kutokuwepo nitalizungumzia katika makala maalum Inshaallah.

Ama katika makala hii tutamzungumzia mwanawachuoni huyu aliyedhulumiwa na Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga Sheikh Salim Barahiyan!

Pamoja na upotoshaji alioufanya sheikh Barahiyan pia aliahidi kuwa atakuja Shk Abu Hamza (aliyekuwa muajiriwa mwenzake katika taasisi ya al muntada al Islamy iliyoko kule UK.) kutoka Mombasa Kenya kuendeleza dhulma hiyo dhidi ya Sheikh huyo (Rabii ).

**Je maulamaa wakubwa wa Sunna wanasema nini kuhusu msimamo wa Sheikh Rabii?**

Tunapowazungumzia maulamaa ni lazima turudi kwa maulamaa, kwasababu wao ndiyo wanaowajua maulamaa wa haki na maulamaa wa batili,hivyo basi katika sehemu hii nitawataja baadhi ya maulamaa wakubwa wa Sunna katika zama hizi na kauli zao kuhusu mwanawachuoni huyu, kisha uamuzi uwe wako ndugu msomaji.

Na kwa hilo utagundua ninani mwenye matatizo
Je Sheikh Rabii au ni waajiriwa wa al Muntada al Islamy ndiyo wenye matatizo?

Mwanawachuoni wa kwanza;

**Amesema Sheikh Ibn Baaz;**
**((الشيخ ربيع من خيرة أهل السنة والجماعة،ومعروف أنه من أهل السنة ومعروف كتابته ومقالاته )).**
((Sheikh Rabii ni mtu wa kheri katika Ahli Sunna wal Jamaa,na ni maarufu kwamba yeye ni katika Ahli Sunna,na vitabu vyake na makala zake pia ni maarufu)).
Tazama kitabu athanaul badi'I uk 13.
Na aliulizwa Sheikh Ibn Baaz kuhusu Sheikh Rabii akasema;
"kuhusiana na masheikh hawa wawili watukufu Sheikh Muhammad Aman al Jaamy,na Sheikh Rabii Ibn Haady al Mad khaly,wote hao wawili ni katika Ahli Sunna na wanafahamika kwetu sisi kuwa ni wenye elimu na fadhila na itikadi iliyo salimika na amefariki Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy usiku wa alhamisi inayo wafikiana na tarehe 27 Shaaban mwaka huu…**basi nina wausia kupata faida kwa kusoma vitabu vyao.."**
Akasema tena;
"Na ndugu zetu masheikh maarufu wa Madina sisi hatuna shaka nao wao wana itikadi nzuri,na ni katika Ahli Sunna wal Jamaa mfano;
Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy,
**Sheikh Rabii Ibn Haady,**
Sheikh Swaleh al Suhaimy…wote hao tuna watambua kwa msimamo mzuri,na elimu na itikadi nzuri…LAKINI WALINGANIZI WA BATILI! Wale wenye kuvua katika maji machafu ndiyo ambao wanataka kuwashawishi watu .."!!
Kitabu athanaaul badi'u uk 13-14.
Huo ndiyo mtazamo wa Ibn Baaz juu ya Sheikh Rabii al Mad khaly! Mko wapi enyi walinganizi wa batili mnao washawishi watu kwamba Rabii kaja na fikra mpya (Salafiyya Jadida)!

**Mwanawachuni wa pili;**

Sheikh Muhammad Naasirud Din al Albany r.a.yeye amesema baada ya kuulizwa swali;

**((على الرغم من موقف فضيلة الشيخين ربيع بن هادي المدخلي ومقبل بن هادي الوادعي فى مجاهدة البدع والأقوال المنحرفة يشكك بعض الشباب فى الشيخين أنهما على الخط السلفي؟**

**فأجاب –رحمه الله -:**

**((نحن بلا شك نحمد الله –عز وجل – أن سخر لهذه الدعوة الصالحة القائمة على الكتاب والسنة على منهج السلف الصالح دعاة عديدين فى مختلف البلاد الإسلامية يقومون بالفرض الكفائي الذي قل من يقوم به فى العالم** الإسلامي اليوم، **فالحط على هذين الشيخين الشيخ ربيع والشيخ مقبل الداعيين إلى الكتاب والسنة،وما كان عليه** السلف الصالح ومحاربة الذين يخالفون هذا المنهج الصحيح هو كما لا يخفىعلى الجميع إنما يصدر من أحد رجلين:

**إما جاهل،أو صاحب هوى.**

**الجاهل يمكن هدايته.....**

**أما صاحب الهوى فليس لنا إليه سبيل،إلا أن يهديه الله –تبارك وتعالى- فهؤلاء الذين ينتقدون الشيخين-كما ذكرنا**

**إما جاهل فيعلَّم،**

**وإما صاحب هوى فيستعاذ بالله من شره ،ونطلب من الله –عز وجل – إما أن يهديه وإما أن يقصم ظهره)).**

Aliulizwa Sheikh Al Bany swali lifuatalo;

"Sheikh pamoja na msimamo waliokuwa nao masheikh wawili Rabii Ibn Haady al Mad khaly,Muq bil Ibn Haady al Mad khaly katika kupambana na Uzushi na kauli zilizo potoka,baadhi ya vijana bado wanatia shaka kwamba masheikh wako katika mstari wa Salafy?

Akajibu kwa kusema;

"sisi bila shaka yoyote tuna mshukuru Allah s.w.t. kwa kuiwekea da'awa hii njema iliyo simama katika kitabu na Sunna juu ya ufahamu wa wema waliotangulia walinganizi wengi katika miji mbalimbali ya kiislam ambao husimama kutekeleza faradhi kifaya jambo ambalo ni wachache wenye kulifanya katika ulimwengu wa kiislamu hii leo.

**Kuwatukana masheikh hawa wawili sheikh Rabii,na Sheikh Muqbil ambao wanalingania kwenye kitabu na Sunna kwa ufahamu wa wema walio tangulia,**na kupambana na wale ambao wanaihalifu hii **manhaji sahihi kama ambavyo haijifichi kwa wote kwamba jambo hili (la kuwatukana) halitoki ila kwa mmoja kati ya watu wa sampuli mbili;**

**IMA MJINGA.**

**AU MTU WA KUFUATA HAWAA(MATAMANIO YAKE)!**

**Jahili kuna uwezekano wa kumuongoza.**

**Ama mwenyekufuata matamanio yake hatuna njia ya kumfanya ila kumuomba Allah amuongoze.**

**Kwahiyo hawa ambao wanawatukana**(1) **hawa masheikh wawili-** kama tangulia kutaja- **mjinga ataelimishwa.na mwenye matamanio ya nafsi** **<u>tunamuomba Allah atulinde na shari yake,ima amuongoze AU AUVUNJE MGONGO WAKE".</u>**
Silsilatul hudaa wan nour cassette namba851/1 swali liliulizwa tarehe 9/7/1416h,na Abul Hassan al Ma'ariby.na kitabu athanaul badi'u uk17-18.

---

(1) Kama BARAHIYAN MUDIR WA A.M.Y.C.alipowaita masheikh hawa kuwa ni SALAFIYYA JADIDA !!!

Amesema tena Sheikh Al Bany;

**قال الإمام العلامة محدث العصر محمد ناصر الدين الألباني:**
**أقول: إن حامل راية الجرح والتعديل اليوم فى العصر الحاضر وبحق هو أخونا الدكتور ربيع،والذين يردون عليه لا يردون بعلم أبداً والعلم معه....**

**Ninasema kwamba;aliyebeba bendera ya Jarhu wa Ta'adil katika zama za leo tena kwa haki ni ndugu yetu Dkt Rabii.Na wale wanaompinga,daima hawampingi kwa elimu,na elimu ipamoja na Rabii..**
**Tazama kitabu at thanaaul badi'u uk 18.**

Na amesema tena sheikh Al Bany alipokuwa akikipongeza kitabu cha Sheikh Rabii kiitwacho "al Qawaaswim" ambacho ndani yake anazibainisha na kuzipinga fikra potofu za Sayyid Qut bi;

**((كل ما رددته على سيد قطب حق وصواب ومنه يتبين لكل قارئ مسلم على شيئ من الثقافة الإسلامية أن سيد قطب لم يكن على معرفة بالإسلام بأصوله وفرعه.**
**فجزاك الله خيراً أيها الأخ الربيع على قيامك بواجب البيان والكشف <u>عن جهله</u> <u>وانحرافه عن الإسلام))</u> !!**

"yote uliyomjibu Sayyid Qut bi ni haki na ni sawasawa,na hapo ndiyo inabainika kwa kila msomaji wa kiislamu ambaye ana maarifa ya kiislamu japo kwa uchache kwa Sayyid Qut bi hakuwa na maarifa ya uislamu katika itikadi wa katika sheria.
Basi Allah akulipe kheri ndugu yetu Rabii kwa kuutekeleza wajibu wa kubainisha na kuuweka **<u>UJINGA WAKE,NA KUPINDA KWAKE KATIKA UISLAMU</u>**".!!!!
Tazama kitabu Baraatu Ulamaail Umma uk 33,na uk 116.

**Mwanawachuoni wa tatu ni;**
Sheikh Muhammad Swaleh Ibn Uthaimin r.a.amesema Sheikh huyo baada ya muhadhara uliotolewa na Sheikh Rabii katika mar kaz yake – sheikh Ibn Uthimin- iliyopo katika mji wa Unayza;

**((إننا نحمد الله سبحانه وتعالى أن ييسر لأخينا الدكتور ربيع بن هادي المدخلي أن يزور هذه المنطقة حتى يعلم من يخفى عليه بعض الأمور أن أخانا وفقنا الله وإياه على جانب السلفية طريق السلف. ولست أعني السلفية أنها حزب قائم يضاد لغيره من المسلمين ،لكني أريد بالسلفية أنه على طريق السلف فى منهجه ...)).**

"hakika sisi tunamshukuru Allah s.w.t.kwa kumfanyia wepesi ndugu yetu Dkt Rabii Ibn Haady al mad khaly kutembelea katika mji huu ili wapate kujua wale ambao hawajui baadhi ya mambo kwamba ndugu yetu –Allah atuwafikishe na yeye pia- yuko katika upande wa Salaf ,njia ya Salaf,
Na sikusudii kwamba Salafiya ni kikundi(chama) kilicho kuwa dhidi ya waislamu,lakini nakusudia Salafiya;njia ya Salaf na MAN HAJ YA SALAF.." maneno haya yanapatikana katika kitabu athaanaul badi'u uk 21.pia katika Cassette iitwayo It'haful kiraam iliyorekodiwa Unayza.

Na aliulizwa Sheikh Ibn Uthaimin swali lifuatalo;
"una toa nasaha gani Sheikh kwa wale watu ambao wanawazuilia watu kusikiliza kanda za Sheikh Rabii kwa madai kwamba zina leta fitna..?

Akajibu sheikh kwa kusema;
**((رأينا أن هذا غلط وخطأ عظيم،والشيخ ربيع من علماء السنة ومن أهل الخير،وعقيدته سليمة ومنهجه قويم .**
**لكن لما كان يتكلم على بعض الرموز عند بعض الناس من المتأخرين وصموه بهذه العيوب!!((**
"nimeona kuwa hili kosa kubwa,na sheikh Rabii ni katika masheikh wa Sunna na katika watu wa kheri na itikadi yake imesalimika na Manhaji yake imenyooka.
Lakini alipoanza kuwasema baadhi ya viongozi wa badhi ya watu wa zama za sasa wakamtia aibu hizi".
Kitabu athanaaul badi'u uk 23.

Huo ndiyo msimamo wa sheikh Ibn Uthaimin juu ya sheikh Rabii na huo ndiyo mtazamo wake wale wote wanao msema vibaya sheikh Rabii.
Sababu kuu ni kwamba sheikh Rabii amemkosoa sheikh wao Sayyid Qutbi ndiyo hili balaa lote lililomshukia !
Athanaaul badi'u uk 23.

**Sheikh wa nne;**
Sheikh Muhammad Ibn Abdillah as Subail Imamu katika msikiti wa Makka;
Aliulizwa sheikh kuhusu wale wenye kuzizuia cassette za sheikh Muhammad Aman Al Jaamy,na sheikh Rabii al Mad khaly kwa madai kwamba zina leta fitna.
Akasema;

**(( أعوذ بالله أعوذ بالله ..لا شوف هذين الشيخين أشرطتهم من أحسن الأشرطة هؤلاء يدعون إلى التمسك بالسنة ولكن ما يتكلم بهؤلاء إلا إنسان صاحب هوى،وأكثر ما يتكلم بهؤلاء أهل الأحزاب الذين ينتمون إلى حزب من الأحزاب هم الذين ينكرون هذه الأشياء أما بالنسبة لهذين الشيخين معروفين بالتمسك بالسنة وعقائدهم سلفية وهم أحسن الناس)). شريط كشف اللثام .1/**

"Audhu billah Audhu billahi…hapana ! angalia hawa masheikh wawili kanda zao ni kanda nzuri zaidi wao wanalingania watu kwenye Sunna na kushikamana na Sunna,lakini hawasemi vibaya masheikh hawa wawili isipokuwa mtu anayefuata matamanio ya nafsi,na wengi kati ya wanao watukana masheikh hawa ni Mahizbi wanaojiunga na vyama wao ndiyo wanaopinga.
Ama kuhuhusu masheikh hawa (sheikh Muhammad al Jaamy,na Rabii) ni maarufu kwa kushikamana na Sunna na ITIKADI YAO NI YA SALAF,nao ni watu wazuri"
Kash fu litham/1.

**Sheikh wa tano;**
Amesema sheikh Zayd Ibn Muhammad al Mad khaly alipokuwa akimjibu Muhammad Surur bosi wa al Muntada al Islamy;

**(( وإنني لأؤكد لمحمد سرور وأعوانه أنه إذا لم يكن الشيخ ربيع بن هادي المدخلي ومشايخه وزملاؤه وتلاميذه على منهج السلف وأتباع الحديث والأثر فلا أدري عن المقصود بالسلفية والسلفيين))** انظر كتاب الإرهاب لزيد بن محمد المدخلي ص 77.

"mimi ninataka kumthibitishia Muhammad Surur na wasaidizi(1) wake kwamba ikiwa Sheikh Rabii na mesheikh wake na rafiki zake na wanafunzi wake hawako katika man haji ya Salaf na wafuasi wa watu wa Hadithi basi sijui niyapi makusudio ya Salafiya wala masalaf".
Tazama kitabu al Ir'haab uk 77.

Na akasema tena sheikh Zayd alipokuwa akizungumzia majibu ya sheikh Rabii aliyomjibu sheikh Abdul Rahman Abdul khaliq;

**((وقد كانت ردود الشيخ ربيع مؤيدة بتقريظ كوكبة من رجال العلم شهدوا للشيخ ربيع بإصابة الحق ووجاهة النقد ووضوح الرد،لإشتمال ما كتب فى الكتابين من الأدلة النقلية والحجج العقلية تنير الطريق وتقوم بها الحجة)) انظر الإرهاب ص 80.**

---

(1) kama vile Barahiyan na waajiriwa wenzake wa al Muntada al Islamy kule U.K.

"Na kwa hakika kabisa yalikuwa majibu ya sheikh Rabii yameungwa mkono kwa kusifiwa na nyota katika watu wa elimu wote wamemshuhudia sheikh Rabii kwa kuipatia haki na muelekeo mzuri wa kukosoa na majibu ya wazi kwa yale ambayo ameyaandika katika vitabu

viwili katika dalili za kunukulu na hoja za kiakili ambazo zinatia itia nuru njia na kusimamisha hoja". Al Ir'haab uk 80.

Maulamaa wa Sunna wa zama hizi waliomsifia sheikh Rabii ni wengi mno na kauli zao ni nyingi mno lakini kwa kutaka kufupisha nitawaja baadhi yao;
6-Sheikh Ubaidillahi al Mubaarak foury katika maulamaa wa kisalaf huko bara Hindi.
7- Sheikh Muq'bil Ibn Haady al waadi'y.
8- Sheikh Muhammad Ibn Abdul wahab al Banna.
9- Sheikh Ahmad Ibn Yahya an Najmy.
10-Sheikh Ally Ibn Naasir al Faqihy.
11-Sheikh Ubayd al Jaabiry.
12-Sheikh Swaleh al Suhaimy.
13-Sheikh Abdul Aziz al Rajihi.
14-Sheikh Jabir Ibn Muhammad alTiib.

**Ni watu wa aina gani wanao mtukana Sheikh Rabii kwa mtazamo wa maulamaa tulio wataja?**

Kwa mujibu wa maneno ya maulamaa hawa wa Ahli Sunna katika zama hizi ni kwamba wale wote wenye kumtukana na kumkejeli, kumtuhumu sheikh Rabii ni watu wa sampuli hizi;

1-Maduati (walinganizi) wa batili.na sababu yao kuu ya kufanya hivyo ni kutaka kuwashawishi watu wasiijue haki! Rejea maneno ya sheikh Ibn Baaz uk 4 katika makala hii.

2-Mtu jahili (mjinga) asiye na elimu na kujua mambo.rejea maneno ya Al Bany uk 5.

3-Mtu mwenye kufuata matamanio ya nafsi yake,na hataki kufuata haki bali na kutetea mas ala binafsi.rejea uk 5.

4-Watu wanaompinga sheikh Rabii wengi wao hawampingi kielimu.rejea maneno ya Al Bany uk 6.

5-Watu wanaompinga Sheikh Rabii kwasababu ya kuwa amewakosoa vigogo wao kama vile Sayyid Qut bi.

6-Mahizbu (watu wa vyama vya bid'a).hawa ni wale wafuasi wa vyama kama vile Ikhwan Muslimin Hizbu tahriri Jamaat tabligh au waathirika

wao na wengi wao ni wale ambao wanajinasibisha na Sunna na kufuata Man haj ya Salaf swalih.

## Sheikh Bakri Abu Zayd na waraka wa dhahabu

Watu wavyama hivyo vya bid'a tulivyo vitaja na watetezi wao wale waliovaa vazi la Sunna na kufuata man haji ya Salaf wanamchukia sana sheikh Rabii kwa dhulma na uadui.
Na sababu ya chuki zao ni kama alivyo tuelezea sheikh Ibn Uthaimin kuwa ni pale sheikh Rabii aliposimama kubainisha uovu na uzushi wa baadhi ya viongozi wao.

Na kwasababu lengo si dini bali ni kufuata hawaa zao wakawa watu hawa wanasubiri ni wapi atateleza Rabii ili wamuumbue ?!

Ninani atakaye simama kumjibu Rabii –japokuwa kwa batili- wamuunge mkono?!
Ni sawa kuna hoja na dalili au kwa dhulma na uadui hilo wao hawalijali ilimradi apatikane mtu atakaye mpinga sheikh huyu na wao wamuunge mkono.

Ndiyo pale ulipotoka waraka ambao Mahizbu wameuita "The Golden letter" barua ya dhahabu !!waraka huu unamkandamiza sheikh Rabii lakini kwa dhulma kama tutakavyoona watu hawa kwasababu ya nia zao mbaya wakautawanya kwa wingi mno,takribani kila pembe ya dunia na kutarjumiwa kwa lugha nyingi! Tena bila idhini ya muandishi!

Hebu tuwasikilize baadhi ya maulamaa wanasema nini kuhusu waraka huu?

Walijitokeza baadhi ya masheikh kumuhoji sheikh Bakri kwanini ameuotoa waraka huu ambao haukujengeka kielimu na insafu?

Aliulizwa swali hilo na sheikh Zayd Ibn Muhammad al Mad khaly sheikh Bakri akawatukana wale wenye kuusambaza waraka huo na kusema hawa wanataka kufarikisha baina ya marafiki wapenzi!!

Alipoulizwa na sheikh Ally Hassan al Halaby-mwanafunzi wa sheikh Al Bany akasema; waraka huu umeibiwa na umetoka bila idhini yangu!

Na sheikh Swaleh al Fawzan pia alimlaumu sheikh Bakri kwa kuutoa waraka huu.

Nayeye sheikh Bakri hajaukana waraka huo wala kuuthibitisha rasmi lakini pamoja na hayo tujaalie kwamba ni wake na umetoka kwa ridhaa yake,lakini je ni ya haki yale yaliyoandikwa ndani ya waraka huu?
na yana upeo gani wa kielimu na insafu?

Kwanza nataka ifahamike kwamba hicho kitabu kilicho andikwa na sheikh Rabii (Adh wau Is laamiya fy aqidat Sayyid Qut bi) ambacho ndani yake kinabainisha itikadi potovu za Sayyid Qut bi.
Kama vile itikadi ya;

a)kwamba Qur'an imeumbwa.
na hii ni itikadi ya watu wa bi'da kama vile; ibadhi,shia,mu'tazila.
Tazama katika katika kitabu chake fi dhilalil Qur'an juz 1 uk 38.

b)anamtukana mtume wa Allah s.w.t. Nabii Mussa a.s kwa kumuita kuwa ni mtu mwenye ukabila !!

tazama kitabu chake at tas'wirul fanny uk 200.

c)hautambui ukhalifa wa Uth'man r.a.
tazama kitabu chake al adalatul ij'timaiyah uk 206.

d)anawatukana maswahaba kama vile Muawiya na Amru bin al asi.
Na kudai kwamba Swahaba Muawiya na Amru Ibn al Aswi wanatumia khiyana uongo na unafiki.
Tazama kitabu chake kutubun wa sha'swiyat uk 242.

e)itikadi yake potofu ya wih'datul wujudi,nayo ni itikadi ya kikafiri ya kwamba kila kitu ni mungu,na mungu ni kila kitu,
Tazama itikadi yake hiyo katika kitabu chake cha tafsiri fi dhilalil Qur'an juz 6 uk 4402,akiifasiri suratul ikhlas,pia tazama maneno ya Shk ibin Uthaimin alipokua akiijibu kauli hii ya upotofu ya Sayyid Qut'bi,tazama majallatud da'awa toleo namba (1591) tarehe 9/1/1418 h.
Sheikh Rabii kabla ya kutoa idhini ya kuchapishwa kitabu hiki alikipeleka kwa maulamaa wengi tena wakubwa kiumri na elimu kuliko sheikh Bakri na hawajayaona aliyo yaona sheikh Bakri.bali baadhi yao wameyasema yale anayo yasema sheikh Rabii kwa mfano;
1- amsema sheikh Al Bany;

**"نقل سيد قطب كلام الصوفية ولايمكن أن يفهم منه إلا أنه يقول بوحدة الوجود".**
**انظر: برآءة علماء الأمة ص 42.**

"Ameyanukulu Sayyid Qut bi maneno ya masufi.na haiwezikani kufahamika maneno hayo ila kuwa Sayyid anasema wih'datul wujuud".
Tazama kitabu baraatu ulaamail umma uk 42.

2-amesema sheikh Ibn Uthaimin;

**"قرأت تفسيره – يعني في ظلال القرآن لسيد قطب- لسورة الإخلاص،وقد قال قولاً عظيماً فيها،مخالفاً لما عليه أهل السنة والجماعة، حيث إن تفسيره لها يدل أنه يقول بوحدة الوجود".**

"Nimeisoma tafsiri yake-Fi dhilalil Qur'an ya Sayyid Qut bi- katika suratil Ikhlas,kwahakika amesema maneno makubwa yenye kuhalifian na yale waliyo nayo Ahli Sunna wal Jamaa.
Kwahakika katika tafsiri yake ya sura hiyo anasema wihdatul wujuud".
Tazama kitabu baraatu ulamail umma uk 42.

Na maneno kama haya ameyasema sheikh Abdallah ad Duwaysh katika kitabu maalumu alichokiandika kwa ajili ya kuzibatilisha itikadi potofu za Sayyid Qut bi zilizomo kwenye tafsiri yake,akakiita kitabu hicho kwa jina la

**(المورد العذب الزلال في التنبيه أخطاء الظلال !!!)**

**"al Mawridul adh bu zulaal fi tan bihi akh taai dhilaal".**
Kwahiyo kauli ya sheikh Bakri aliyosema;

**(ومن العناوين الإستفزازية قولكم: (قول سيد قطب بوحدة الوجود ...)**

"na miongoni mwa anuani za kuamsha hisia ni kauli yako(Rabii uliposema);
Kauli ya Sayyid Qut bi ya wihdatul wujuud".

Haikujengeka kielimu kwasababu jambo hili hakulisema Rabii peke yake na wala hakumzulia,bali huo ndiyo mtazamo wa maulamaa wakubwa kuliko sheikh Bakri na Ibn Jibrin,tena maulamaa wakubwa katika mambo ya itikadi watambuzi wa maneno ya watu wa bid'a.

Na sihivyo tu bali sheikh Rabii alipokuwa akimtoa makosa Sayyid ametoa ushahidi wa kutosha juu ya madai yake na hakusema maneno matupu.
Kwa uthibitisho zaidi rejea vitabu vifuatavyo;

1- Adh waau Islaamiyya cha sheikh Rabii al madkhly.

2- al Haddul faasil bainal Haqi wal baatili.pia cha sheikh Rabii,na kitabu hiki ni jawabu ya huo waraka uitwao wa dhahabu.

3-Baraatu ulamail umma,kitabu cha sheikh Isam Ibn Abdillah as Sinany,na kimepitiwa na sheikh Ibnu Uthaimin na sheikh Swaleh al Fawzan.
Ndani ya kitabu hiki kuna jawabu za kutosha juu ya maneno ya sheikh Ibn Jibrin kuhusu uombezi wa sheikh Ibn kumuombea Sayyid Qut bi, na pia kuna jawabu dhidi ya sheikh Bakri na waraka wake huo uitwao na kina Barahiyan kuwa ni wa dhahabu.
Copy za barua za masheikh zinazo msifia sheikh Rabii.

4- al Ir hab cha sheikh zayd Ibn Muhammad Ibn Haady al Mad khaly. Pia mwenye kitabu hiki amemjibu sheikh Abdallah Ibn Abdil Rahman Ibn Jibrin kwa muhatasari kwa kumuunga kwake mkono sheikh Bakri na waraka wake.kama ilivyo katika kitabu hicho uk 85-93.

5-al Aj wibatul mufidah.kitabu kilicho kusanya fatawa za Sheikh Swaleh Ibn Fawzan Ibn Abdillah al Fawzan juu ya mapote ya zama hizi na waanzilishi wake,fatawa hizo zime kusanywa na Jamaal Ibn Furayhan al Haarithy.

## Barahiyan na Salafiyya Jadidah !!

Kama nilivyo tangulia kusema kwamba nina azma ya kuandika makala maalumu kuhusu Salafiyya Jadida na kuyabatilisha maneno ya uongo yaliyotolewa na Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga sheikh Salim Abdur Rahim Barahiyan.

Si vibaya hapa kuyagusia kidogo yale niliyo kuwa nimeazimia kuyasema kwanjia ya kuhoji,na hapa nina hoji kama ifuatavyo;

Mudir huyo wa Taasisi hiyo tuliyoitaja amesema kwa uwazi kabisa kwamba kuna pote potovu linaloitwa Salafiyya Jadida.kisha akawataja waanzilishi wa pote hilo,akamtaja sheikh Rabii Ibn Haady al Mad khaly kuwa yeye ndiye muanzilishi namba moja wa pote hilo!

Swali
1-Ni kwa fikra zipi ngeni na itikadi zipi potofu ambazo hazikufahamika na maulamaa waliomsifu k.v.
Ibn Baaz,Al Bany Ibn Uthaimin,Fawzan na wengineo tulio wataja hapo nyuma.
Mpaka hii leo akaja kuligundua hilo Salim Barahiyan?

Au ni fikra za kurithishwa kutoka makao ya al Muntada al Islamy London?
Maana hizi ni fikra za Muhammad Surur ambaye yeye ni katika maulamaa na waanzilishi wa al Muntada taasisi iliyo muajiri Mudir wa A.M.Y.C.na ushahidi ni pale aliposema katika kitabu chake al Salafiyyah baina al wulaat wal Ghulaat uk 15;

**(هذه الإكتشافات الخطيرة التي انفرد بها المدخلي وأعضاء حزبه ...!!!..)**

Amesema sheikh huyo wa al Muntada;
"na huu ni uvumbuzi mpya na wa hatari uvumbuzi ambao amepwekeka nao al Mad khaly na CHAMA chake…"

Hizi ndizo fikra za Muhammad Surur dhidi ya sheikh Rabii! Na hii ndiyo athari mbaya za kuajiriwa na Taasisi zilizo na fikra potofu matokeo yake ni haya,Boss akituhumu nawe watuhumu! Basi bila ya elimu wala hoja?

Na maswali mengine yatafuatia katika makala maalumu itakayo zungumzia "Salafiyya Jadida".

## khatima

mwisho nina khitimisha makala hii kwa kuiusia nafsi yangu kwanza kumcha Mungu.
Pia kumuusia Mudir wa A.M.Y.C. Sheikh Salim Barahiyan ucha Mungu na anapo zungumza basi azungumze kwa elimu au anyamaze, na pia kuwa mkweli katika mazungumzo yake na kuacha propaganda -kama ilivyo kawaida katika mihadhara yake-

Na pia ufahamu kwamba maneno uliyoyazungumza kuhusu sheikh Rabii, na sheikh Muq'bil ni maneno makubwa tena ya dhulma dhidi yao.
Na hili linawashangaza watu wa Sunna walio katika man haji sahihi ya Salaf !
Vipi mtu anadai yuko katika man haji sahihi anawatetea wazushi kama Sayyid Qut bi na Hassan al Banna, na kuwakandamiza maulamaa wa Sunna kama vile sheikh Rabii,Muq'bil na sheikh Yahya al Hajuury tena hawa ni ulamaa wa Sunna kwa ushuhuda wa maulamaa wa Sunna?!

Kwa faida zaidi fuatilia mfululizo wa makala zetu hizi;

-Upambanuzi juu ya hukumu ya picha.

**-Mjue imamu wa Jarhu wat taadili katika zama hizi Rabii al Mad khaly** .
ambayo ndiyo hii iliyoko mikononi mwako.

Mjue Imam wa Hadithi wa Yemen katika zama hizi Muq bil al Waady .

Ni kina nani Salafiy Jadida?

Itikadi za Sayyid Qutbi na Hassan al Banna kwa mtazamo wa sheria.

Ikh wanul muslimina katika mizani ya Sunna.

**Nb;**
**ukiipata makala hii toa copy nyingine ili kueneza ujumbe,Allah atakupa ujira wa kutangaza kheri.**

**وبالله التوفيق**

**وصلى الله وسلم وبارك على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين**